Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 02 Issue: 01 | April - 2023

EAJK

# Itikadi Kuhusu Jinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa katika Kaunti ya Bomet, Nchini Kenya

**Authors**
**Nancy Kones** [(1)]; **Abdulrahim Hussein Taib Ali** [(2)]; **Mayaka Gwachi** [(3)]
**Main author email:** konesnancy2013@gmail.com

**(1.2) Egerton University, Kenya; (3) Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Kones, N., Ali, A. H. T., & Gwachi, M. (2023). Itikadi kuhusu jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika kaunti ya Bomet, nchini Kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 2*(1), 95-106. https://doi.org/10.51317/eajk.v2i1.345

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 20.02.2023
Accepted: 17.03.2023
Published: 14.04.2023

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2023 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Utafiti huu ulishughulikia itikadi kuhusu jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Ulichunguza kama nyimbo za kampeni za kisiasa zilichangia kuchaguliwa kwa wanawake wachache kuliko wanaume katika uchaguzi mkuu. Lengo mahususi la utafiti huu lilikuwa kufasili jinsi nyimbo za kampeni za kisiasa hueleza suala la itikadi kuhusu jinsia. Utafiti huu uliegemea nadharia ya Ubabedume. Huu ni utafiti wa kithamano mkabala wa kifasili. Mtafiti alizikusanya nyimbo hamsini na mbili za kisiasa ambazo zilikuwa zimerekodiwa katika kanda. Sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteua nyimbo ishirini na mbili za kampeni za kisiasa ambazo zilikuwa zinaambatana na jinsia. Wasanii kumi na sita waliimba nyimbo hizo ambazo zikawa deta za kuchanganuliwa. Mtafiti alikusanya deta kwa kuzisikiliza kanda za nyimbo na kutumia mwongozo wa maswali ya mahojiano. Alitumia mbinu ya ufasili wa deta katika utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba wagombezi wa kiume walipewa uwezo, hadhi ya juu na mamlaka hasa kulingana na nguvu zao za kimwili. Mtafiti apendekeza kwamba utafiti zaidi ufanywe kuchunguza namna ya kusawasisha uwezo wa mwanaume na mwanamke kupitia vyombo vingine vya kijamii.

**Maneno muhimu:** Itikadi, Jinsia, Nyimbo za kampeni za kisiasa.

**UTANGULIZI**

Nyimbo hutumika kama hifadhi au rekodi za matukio muhimu ya kihistoria katika jamii (Wamitila, 2008). Nyimbo za kampeni za kisiasa hutumika wakati wa uchaguzi mkuu nchini Kenya. Wachaguliwao ni rais, magavana, maseneta, wabunge, wawakilishi wa wanawake na wajumbe wa wadi. Utafiti ulichunguza kama nyimbo za kampeni za kisiasa zilichangia kuchaguliwa kwa wanawake wachache kuliko wanaume katika uchaguzi mkuu.

Simatei (2010) aeleza kwamba mipango ya kijamii na kisiasa, baada ya siasa ya vyama vingi nchini Kenya mwaka wa 1992, ilileta ubunifu mwingi katika uwanja wa usanii hasa katika utanzu wa nyimbo. Mwaka wa uchaguzi wa 2002, kulizuka aina nyingi za muziki wa kisiasa kutoka makabila mbalimbali. Nchini Kenya, nyimbo za kisiasa zimetumika kuelimisha watu kabla na baada ya uhuru. Siasa ni dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa uendeshaji wa masuala ya kijamii katika taifa. Siasa inaweza kutumika kuelezea mahusiano kati ya makundi mbalimbali kama vile siasa ya kijinsia.

Wamitila (2003) atufahamisha kwamba maudhui yapatikanayo katika nyimbo teule za kampeni za kisiasa ndiyo yale yanayopatikana katika jamii nyingi za Kiafrika hasa zile ambazo zina kiwango kikubwa cha mfumodume. Kutokana na mfumodume, wanawake wengi wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza na kujikomboa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kutokana na hadhi ya mwanamke kuwa chini ikilinganishwa na mwanaume, taswira ya mwanamke inayopatikana katika misemo, nyimbo na kazi nyingi za kifasihi zimedhihirisha udogo wa mwanamke. Tendo la mwanaume linakuwa na mwelekeo chanya na la mwanamke linaleta sifa hasi.

Mnamo 2002, shughuli za kisiasa zilitajwa kuwa za haki na huru na Jamii ya Kimataifa. Kukazuka makundi mengi maarufu ya wanawake. Malengo yao mahususi yalikuwa kuelimisha jamii kuhusu uwezo wa wanawake siasani, uimarishaji wa wanawake wagombezi na wapigaji kura, na elimu kuhusu usawa wa jinsia. Wanawake washindi katika uchaguzi huo walikuwa pamoja na Charity Ngilu, Beth Mugo na Martha Karua. Serikali mpya ilipoundwa mwezi Machi 2003, uwakilishi wa wanawake katika idara ya serikali ilikuwa hivi: Baraza la Mawaziri: wanawake watatu kwa wanaume ishirini na watatu, Manaibu wa Mawaziri: wanawake wanne kwa wanaume ishirini na wanne, Makatibu wa kudumu: wanawake tisa kwa wanaume ishirini na wanne na Wakurugenzi wa idara: wanawake watatu kwa wanaume ishirini na saba.

Uchaguzi wa 2007, mshindi alikuwa Mwai Kibaki wa chama cha PNU na wa pili alikuwa Raila Odinga wa chama cha ODM. Nazlin Umar katika chama cha WCP of Kenya alikuwa wa sita. Wanawake wabunge waliongezeka hadi ishirini na mmoja kati yao kumi na watano waliochaguliwa na sita walioteuliwa.

Uchaguzi wa kitaifa wa 2013 ulifanywa chini ya katiba mpya iliyopitishwa 2010. Huu ni uchaguzi ulioshughulikiwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Kulingana na IEBC, Uhuru Kenyatta wa Muungano wa Jubilee aliongoza na Raila Odinga wa CORD alikuwa wa pili. Martha Karua wa NARC-Kenya, kwa wagombea wanane, alikuwa namba sita (Commonwealth Observer Group, 2013). Katika bunge, wanaume mia mbili na tisini na wanawake kumi na sita walichaguliwa.

Uchaguzi wa kitaifa wa 2017, Uhuru Kenyatta wa Muungano wa Jubilee alikuwa wa kwanza na Raila Odinga wa Muungano wa NASA, alichukua nafasi ya pili. Hakukuwa na mwanamke aliyegombea kiti cha urais. Magavana wa kike watatu walichaguliwa kwa mara ya kwanza nchini kama ifuatavyo: Charity Ngilu kutoka Kaunti ya Kitui, Ann Waiguru kutoka Kaunti ya Kirinyaga na marehemu Dkt. Joyce Laboso kutoka Kaunti ya Bomet. Vilevile, maseneta wa kike watatu walichaguliwa kwa mara ya kwanza kama ifuatavyo: Margaret Kamar wa Kaunti ya Uasin Gishu, Susan Kihika wa Kaunti ya Nakuru na Fatuma Dullo wa Kaunti ya Isiolo. Katika bunge la kitaifa, wanawake walikuwa arubaini na saba kwa mia mbili themanini na tisa. Baada ya kila uchaguzi, wabunge kumi na wawili huteuliwa kutoka makundi matatu maalumu, yaani, kundi la vijana, la walemavu na la wanawake. Wao huchukuliwa kama watu wasioweza kushindana kwa usawa na wagombezi wengine.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Itikadi ya Kisiasa kwa Jinsia ya Kiume**

Connell na Messerschmidt (2005:832) waeleza kwamba nadharia ya Ubabedume huhitaji wanaume kujihusisha nao na huhalalisha kiitikadi wanaume

kuwatawala wanawake duniani. Deacon na wengine (1999) waeleza kwamba ni muhimu kutaja kuwa desturi za kijamii na mahusiano ya wanajamii huundwa kutokana na raghba ya mtazamo na dhana mahususi mintarafu ya uhalisi wa kijamii.

Marion Chelang'at ambaye alikuwa akitetea Muungano wa Jubilee, alijitahidi kuwashikamanisha watu ili wawe na umoja. Alielewa kwamba wanachama wa Muungano wa Jubilee wangepata wapiga kura wengi iwapo watu wangeungana kwani umoja ni nguvu. Muungano wa Jubilee uliundwa na wanaume wengi na wanawake wachache mno. Kulingana na wimbo huu, uchinjaji wa ng'ombe hufanywa na wanaume kuonyesha kwamba Muungano huo wa Jubilee ulitawaliwa na wanaume. Hili ni dhihirisho kwamba bado jinsia ya kiume ina uwezo mkubwa kisiasa kuliko ya kike katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kokiyonjine kiy.*
*Kiyenye tany ak kepchei.*
*Kole alak moche chatit.*
*Kole alak moche chatit akichek.*
*Kyome tugul en konyon.*

*Tumeamua kubaliano la siri.*
*Tutachinja ng'ombe na tuigawe.*
*Wengine wanasema wanataka paja.*
*Wengine wanataka paja pia.*
*Tutakula sisi sote katika nyumba yetu.*

Izugbara (2005) aeleza kwamba chimbuko la nadharia ya Ubabedume hufungamanishwa na dhakari na wenye kuimiliki, yaani, wanaume. Wanachukuliwa kuwa na nguvu na wa kuheshimika katika jamii. Siku zote mwenye dhakari hupewa hadhi ya juu na kuchukuliwa kuwa bora zaidi ya wale ambao hawana kiungo hiki, yaani, wanawake. Uhusiano baina ya mwanamke na mwanaume umejengwa katika mazingira yanayotukuza ukuu wa wanaume na udogo wa wanawake katika jamii.

Kupitia wimbo ulioimbwa na Jeremiah Kosgei, Samoei Ruto anaheshimiwa na jamii ya Wakalenjin kama kiongozi wao kwa kuitwa baba. Ruto alitumwa ampeleke Uhuru kutawazwa ili afanikiwe katika kinyang'anyiro cha kiti cha urais. Uhuru alifananishwa na Mfalme Daudi mwana wa Jesse katika Bibilia. Mfalme Daudi alikuwa mwenye nguvu kupindukia na aliheshimika sana kupitia matendo yake. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kokiyokten bamong'o Arap Ruto.*
*Imutwech Uhuru konyo Kapkatet.*
*Si kikochin mwaita nebo Kalenjin.*
*Kou weritab Jesse nemi Bible.*

*Tunakutuma baba yetu Arap Ruto.*
*Utuleteee Uhuru aje Kapkatet.*
*Ili tumtawaze kwa mafuta ya Kalenjin.*
*Kama mwana wa Jesse katika Biblia.*

Aswani na wengine (2014) waeleza kuwa uwezo, itikadi, majukumu na mamlaka ni masuala yanayobainisha mahusiana na utofauti na hasa zaidi athari ya tofauti hizi katika mfumo wa jamii. Wimbo ulioimbwa na Jeremiah Kosgei, unaeleza kwamba Ruto ni shujaa awezaye kumwua simba anayenguruma na hakuna adui anayemweza. Yeyote aliye mamlakani, anapaswa kuwa shujaa na mwenye uwezo mkubwa wa kumwezesha kuongoza kulingana na sehemu hii ya wimbo.

*Kongoi nyiganet.*
*Bar ng'etuny korose.*
*Kogerin bunyon koimen.*
*Iger inye kolaba.*

*Asante shujaa.*
*Amwuaye simba akiwa ananguruma.*
*Adui akikuona kunakuwa giza.*
*Ukimwona kunakuwa mwangaza.*

Kosgei alimhimiza Ruto arudishe utawala kwa jamii ya Kalenjin wakati Uhuru atakapohitimisha kipindi chake cha utawala. Tendo hili linaonyesha jinsi jinsia ya kiume inasawirika kuwa na mamlaka. Hii ni itikadi inayoleta udumishaji wa ubabedume katika jamii. Fairclough (1989) abainisha mikakati maalumu ya uchanganuzi wa lugha mintarafu ya mahusiano na uwezo, itikadi na mabadiliko ya jamii na utamaduni. Aeleza kwamba kutokana na urudiaji usioepukika katika utamaduni mzima, itikadi mwishowe hufanywa kuonekana kuwa suala la kiasili na ina nafasi yake maalumu katika mchakato mzima wa kujenga ubabedume. Usemi au matini ni sehemu ya mapambano ya kubainisha tofauti katika itikadi, mamlaka na uwezo unaobainisha

mvutano wa kiutawala baina ya jinsia ya kiume na ya kike. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Wegun tuga ak irib en kaptich.*
*Bokokyin Uhuru kotwoisiok.*
*Si ngemi tai kotililit sumenyon.*

*Warudishe ng'ombe na uwachunge zizini.*
*Umwachie Uhuru atimize.*
*Halafu tuwe na muungano mwema mbeleni.*

Macleunness (1998) afafanua kwamba udume hauwezi kubainishwa kama sifa ya mwanaume bali hutokana na itikadi na utamaduni wa jamii husika. Masharti mahususi ya kihistoria yanayothibiti imani za mume na mke katika jamii na majukumu yao tofauti huendelezwa kupitia kwa imani za jamii, matarajio na mielekeo yao. Ruto kama mwanaume, anashauriwa na Kosgei kwamba hekima ni uwezo. Alimwarifu kuwa yeye ni baba ya Wakalenjin, ndume ambaye amewekwa pembeni. Maelezo haya yanabainika katika sehemu hii ya wimbo.

*Kimnotet naet we Samoei.*
*Kongoi kirginyon.*
*Kongoi kipwalei kipken bun.*
*Kitienge en tobonik we babanyon.*
*Kikamwa boiyon kiba kel belyon.*
*Kibendi mochei keldo.*

*Samoei akili ni mali.*
*Asante ndume yetu.*
*Asante mweza adui.*
*Baba yetu tunakutegemea pembeni.*
*Mhenga alisema kutakuwa na fanaka.*
*Pole pole ndio mwendo.*

Vilevile, Shuttle Sisters ni wasanii ambao walidhihirisha maelezo tuliyopewa na Maclenness (1998) katika wimbo wao. Walifafanua kwamba Samoei ni mwanaume anayetambulika katika nchi nzima ya Kenya kwa kuwa na nguvu ya kutawala akipata nafasi. Aliombewa na wasanii kuwa rais wa nchi ya Kenya wakati mmoja. Walimhimiza afuate nyayo za Mstaafu Rais Moi kutoka jamii ya Wakalenjin aliyetawala nchi ya Kenya kwa miaka kadhaa. Wimbo huu unashamiri ujengaji wa ubabedume katika jamii ya Wakalenjin. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Mami bororiet Kenya ne moingen kainetab Samoei.*
*Kisaun kot indochi emenyon Kenya.*
*Ye indochi emenyon, ibur kou Baba Moi.*

*Hakuna jamii nchini Kenya isiyolitambua jina la Samoei.*
*Tunakuombea hadi uongoze nchi yetu ya Kenya.*
*Utakapo ongoza nchi yetu ukae kama Baba Moi.*

Marion Chelang'at alikuwa na wazo kama hili katika wimbo wake. Alieleza kwamba wanaye mwanaume ambaye ni kifungua mimba anayewaunga wengine mkono siasani ili hata yeye aungwe mkono siku za usoni. Wenyeji wanamwita fahali ainuaye mlima na ni yule akinena, husikilizwa. Jamii ya Wakalenjin hutarajia mwanaume kuwa na nguvu ya kipekee ya kutawala na anapewa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kitindoi taitanyon.*
*Kole robe morik,*
*Si tun ketilji.*
*Kole neranik, chepyosok koboto, boisiek, i kirginyon kipkeleny tulwo.*
*Kirginyon ne ingosil ke yepchin it.*

*Tunaye kifungua mimba wetu.*
*Alisema anaungana mkono,*
*Kusudi aungwe mkono baadaye.*
*Vijana, kina mama na wazee walisema, wewe ni fahali yetu ainuaye mlima.*
*Fahali yetu ambaye akilia hutegewa.*

Fiske na wengine (1987) wanaangaza masimulizi ya matukio hatari, ushari wa vitendo na mashindano sambamba na wanasesere wa kiume. Utamaduni na mazingira huwa vigezo muhimu katika kukuza ubabedume ambao hukolea katika fahamu za wanajamii. Ubabedume unadhihirika katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Kipkurui Ng'eny. Alimhimiza Ruto asimame imara katika siasa na awe kiongozi wa jamii ya Wakalenjin. Awachunge wanaoteseka na awe baba ya mayatima. Kulingana na itikadi na utamaduni ya Wakalenjin, jinsia ya kiume huhusishwa na mambo makuu na huonekana kama mweza yote. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Telel Arap Ruto nyiganetab Kalenjin.*
*Ribwech che seretos.*
*Ribwech che motindo sigik.*

*Iweiigu babanyuan.*
*Indochin bikab Kalenjin.*

*Simama imara shujaa wetu wa Kalenjin.*
*Utuchungie wanaoteseka.*
*Utuchungie mayatima.*
*Uwe baba yao.*
*Uwaongoze jamii ya Wakalenjin.*

Carrigan na wengine (1985) wafahamisha kwamba Patricia Sexton alitufafanulia kwamba kanuni za jinsia ya kiume zinasisitiza sifa kama vile ujasiri, mwelekeo wa kibinafsi, ubingwa, ustadi wa kiufundi na ugumu katika akili na mwili. Wazo kama hili linasawirika katika wimbo wa msanii aitwaye Ras Wageni. Alikuwa akimwunga mkono Isaac Ruto aliyegombea kiti cha ugavana mara ya pili katika Kaunti ya Bomet. Kupitia wimbo wa Ras, wenyeji walifurahia Isaac Ruto, fahali yao aliye jasiri, ambaye alikiunda chama cha Mashinani. Walimpongeza kwa kuungana na wananchi wa Kenya na kuwatetea watu wa Mau katika tatizo la shamba hadi wakapata haki yao kwani yeye hawezi kushtuliwa na chochote. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kisime echek en chamaitab Mashinani.*
*Kongoi kirginyon.*
*Ingosil koitu tuguk gaa.*
*Kiiyan otononse ak bikab Kenya komugul.*
*Kongoi nyiganenyon Isaac Ruto.*
*Kin itweku konyorchige imanda bikab Mau.*
*Magimuenen magatet.*

*Tunashabikia chama chetu cha Mashinani.*
*Asante fahali yetu.*
*Akilia, mali yanafika nyumbani.*
*Umekubali kusimama na watu wote wa Kenya.*
*Asante shujaa wetu Isaac Ruto.*
*Uliponena, watu wa Mau walipata haki yao.*
*Hushtuliwi kwa ngozi.*

Connell (1987) afafanua kwamba ubabedume, wazo la kimsingi katika maandishi ya Gramsci na mchango mkubwa wa mawazo ya Umaksi, ni kuhusu ushindi na umilikaji wa mamlaka na uundaji (na uharibifu) wa vikundi vya kijamii katika mchakato huo. Ni hasa kuhusu namna ambavyo tabaka la utawala huanzisha na kudumisha utawala huo. Ubabedume huhusu ushawishi wa idadi kubwa ya watu hasa kupitia vyombo vya habari na shirika la taasisi ya kijamii kwa njia zinazoonekana kuwa "kawaida". Ras ni Mwimbaji ambaye alimtaja Isaac Ruto kuwa baba yao aliyeunda chama cha Mashinani ambacho kimeunganisha jamii ya Wakalenjin. Alieleza kwamba tangu Ruto awe gavana wa Kaunti ya Bomet 2013, kazi kubwa ambayo amewafanyia wenyeji imetambulika. Msanii aliwashawishi wenyeji wampigie tena kura 2017 kwani si ungwana kujikinga chini ya mti kukinyesha halafu mvua iishapo, uukate mti huo. Kuna mambo matatu yaliyodhihirika katika wimbo huu kama yafuatayo: Uundaji wa utawala, udumishaji wa utawala huo na ujengaji wa ubabedume katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kongoi en chamainyon.*
*Kongoi babanyon.*
*Mokiyumen sosur ye moen keyeb.*
*Kikotok boisionik tugul chebo kandoindenyon Isaac Ruto.*
*Koiyumenech bik tugul chebo Kalenjin chamainyin nebo CCM.*

*Tunashukuru kwa chama chetu.*
*Tunashukuru baba wetu.*
*Haifai kujikinga chini ya mti kukinyesha, halafu mvua ikiisha uukate.*
*Kazi yote ambayo Isaac Ruto ameifanya, imeonekana*
*Kalenjin wote wameunganishwa katika chama chake cha CCM.*

Waimbaji waliojiita Chama Cha Mashinani (CCM) Women walionyesha maelezo tuliyopewa na Connell. Walifahamisha kwamba Ruto ni shujaa mfano wa moto ambaye ameimarisha maendeleo katika Kaunti ya Bomet hadi ikagundulika kote nchini Kenya. Amewahi kuwa mwenyekiti wa magavana wote nchini Kenya akiwa na umri mdogo. Yeye hana mapendeleo na ameweza kuongoza kaunti yake ipasavyo. Walieleza kuwa malumbano ya kisiasa yanahitaji walio na ujasiri mwingi kama yeye. Waliwasihi wenyeji wamchague yeye tena kuwa gavana kwani ni mwanaume anayestahili kuwa kiongozi. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kiribwech kounti Arap Ruto.*
*Kot kegas en Kenya.*
*Kigoik chairman Arap Ruto en 47.*
*Boiboyet ne tiana yon kiketyi kora Arap  Ruto?*
*Motinye kolotunet Arap Ruto.*

*Ngokerin bunyon koimen,*
*Iger kolaba.*
*Nyoljin kandoinatet.*
*Kongoi we kipkutuny si koet Bomenyon.*
*Kimoitos ra tugul ne moche Nyigonik.*
*Kongoi we nyiganet neu mat.*

*Arap Ruto ametulindia Kaunti.*
*Ikasikika nchini Kenya.*
*Amewahi kuwa mwenyekiti akiwa na Miaka 47.*
*Ni furaha iliyoje Arap Ruto akirudishwa tena?*
*Arap Ruto hana mapendeleo.*
*Adui akikuona kunakuwa giza,*
*Ukimwona kunakuwa na mwangaza.*
*Unastahili kuwa kiongozi.*
*Asante kipkutuny apate kulinda Bomet.*
*Uongozi huu unang'ang'aniwa na wengi na unahitaji mashujaa.*
*Asante shujaa kama moto.*

Connell (1983, 236, 255, 256) anaeleza kuhusu makundi yanayohusika zaidi na uundaji wa itikadi za kijinsia. Ni kweli kwamba makundi haya na udikteta wao husababisha kwa kishindo ugomvi, utawala na miundo ya kikatili ya taasubi za kiume. Kwa ujumla, wale wanaohusika zaidi inaaminika kuwa ni: mapadri, waandishi wa habari, watangazaji, wanasiasa, wanasaikolijia, watengenezaji wa filamu, waigizaji, waandishi wa riwaya, makocha wa michezo na wasomi. Watu hawa wanaendeleza utawala wa kijinsia, tajriba zifaazo, mitazamo; kutafakari na kufasiri mahusiano ya kijinsia. Itikadi za jinsia ya kiume zinadhihirika katika wimbo ulioimbwa na Chama Cha Mashinani (CCM) Women. Walimtaja Ruto kama fahali, shujaa kama moto, kiongozi, mwelekezi, mwenye roho safi, mnenaji, baba yao na mfanyikazi maarufu nchini Kenya. Maelezo hayo yote kupitia wimbo wao, waliwasihi wenyeji kuwa Ruto angebaki kuwa gavana wao tena. Wimbo huu umedhihirisha kwamba waimbaji wa jinsia ya kike huunda utawala wa taasubi za kiume katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kongoi kirginyon.*
*Mokichomndoi kesilwech.*
*Kichome nyiganet neu mat.*
*Kongoi Kimurany ne motinye kolotunet.*
*Kichome Koterkut.*
*Kikotok boisienyin.*
*Kongoi babanyon ne kikenai en Kenya.*
*Mokiwole kora.*
*Ne kikondochi gavanaek.*

*Asante fahali yetu.*
*Haturuhusu aumizwe.*
*Twampenda shujaa mfano wa moto.*
*Asante Kimurany asiye na mapendeleo.*
*Twapenda Koterkut.*
*Kazi yake imeonekana*
*Asante baba yetu aliyejulikana nchini Kenya.*
*Haibadilishwi tena.*
*Aliyewaongoza magavana.*

Sattel (1983:119-124) anahisi kwamba chanzo cha kuelewa ubabedume huhusika na utawala wa hadhi ya juu ya kiume katika jamii. Upendeleo wa jinsia ya kiume na ukuu wao kwa wanawake, kuambatana na uchunguzi wa Sattel, inaendelezwa katika jamii nyingi za Nijeria. Tofauti ya kijinsia katika tamaduni za jamii za Nijeria, huruhusu uwezo na hadhi ya juu kuliko wanawake. Wanaume ni wafalme na viongozi wanaongoza katika kila jambo hata kama maamuzi yao haifaidi jamii. Mawazo haya yanasawirika katika wimbo wa msanii aliyejiita Hotstar Kutundetunde aliyekuwa akimwunga mkono Isaac Ruto. Mwimbaji alifafanua kwamba Ruto ambaye ni jasiri na anawapenda watu wote, atabaki kuwa gavana tena kwani yeye ni mashuhuri. Alieleza kuwa wenyeji wote wamemwunga mkono awe gavana yao tena. Wazee wa kiume ambao wameeleza kwamba wamefaidika kutokana na uongozi wa Ruto, wamembariki yeye apate kuongoza kaunti ipasavyo kama Musa katika Biblia. Musa alipogonga maji kwa fimbo aliyokuwa nayo, maji yakatawanyika na Wayaudi wakavuka. Wazee walimshauri mgombezi pamoja na wenyeji wawe watu wenye busara wasiotaka vita ili wafaulu katika kaunti yao. Kulingana na maelezo ya wimbo huu, ubabedume unaendelezwa katika jamii ya Wakalenjin. Wanaume wanaamua karibu kila kitu kwani ndio wao wanatoa mawaidha yote. Wao hasa waliamua kwamba hawataki gavana mwingine ndipo walimsifu na kumbariki mgombezi. Walieleza namna wamenufaika na kushauri wenyeji kuepukana na vita. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Mokiwole Isaac Ruto.*
*Kisimchini nyiganenyon.*
*Mwoe boisiek, chepyosok ak vjana mokiwole.*
*Mie mugulel.*

*Ki kokonin kirokto boisiek neu nikibo*
*Musa si kelanda.*
*Okot ne iwerto en oret kongenin.*
*Keikun bik che utoten, che mobo boriot.*
*Okot echek boisiek kemi komie.*

*Isaac Ruto habadilishwi.*
*Tunashabikia shujaa wetu.*
*Wazee, kina mama na vijana wanasema haibadilishwi*
*Ana roho safi.*
*Wazee wamekupatia fimbo kama ile ya*
*Musa ili tuvuke.*
*Hata mpitanjia anakutambua.*
*Tuwe watu wenye busara, wasio wa vita.*
*Hata sisi wazee tuko salama.*

Carrigan na wengine (1985) waeleza kwamba ubabedume ni suala la jinsi makundi fulani ya wanaume humiliki mamlaka na utajiri na namna wanahalalisha na kuendeleza utawala wao. Kutokana na ubabedume, wanaume wengi hufaidika kwa kuwatawala wanawake. Kwa wanaume wengine, huwawezesha kutawala wanaume wenzao. Maelezo haya yanasawirika katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Arumutik Kosgei.

Alimtetea Lesan aliyekuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet. Lesan alikuwa amechaguliwa kuwa seneta kuanzia 2013. Alikuwa akigombea kiti hicho mara ya pili. Msanii alifahamisha kuwa kaunti yao inahitaji mtaalamu ambaye angeiimarisha. Lesan alikuwa amebarikiwa na wazee wa kiume kuwa seneta na alitarajiwa kukitumia kiti hicho ipasavyo ili wanaume wengine chipukizi waje wakitumie siku za usoni. Mwimbaji alimshaua Lesan kwa kueleza kwamba yeye ni shujaa ambaye ni ngao na macho ya wenyeji. Yeye hawezi kutishwa wala kutingishika na taa yake inawaka usiku na mchana. Mgombezi alitajika kuwa jasiri wa kukinga pembeni. Alihimizwa na msanii awatatulie wenyeji matatizo kama vile Yusufu na Musa waliwalisha Wayaudi jinsi ilivyoelezwa katika Biblia. Mwimbaji aliwaelezea wenyeji kuwa maelewano, amani na urafiki ni muhimu na kwamba jamii ya Wakalenjin huongozwa na ngao na amri za mababu zetu tangu enzi. Jambo hili likitimizika, wanaume wengine watawaheshimu. Kupitia maelezo ya wimbo huu, mambo yote yamepangwa na jinsia ya kiume kwani imepewa hadhi ya juu na uwezo wa kutawala. Jinsia ya kike ilifichika katika wimbo huu kuonyesha kwamba jamii imeipa hadhi ya chini na imeshamirika kutokuwa na uwezo wa kutoa uamuzi. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Asi ketech Bomet Kounti bo kolili komoche chito ne somanat.*
*Somananing'ung professor ko sobunitab*
*Bomet Kounti.*
*Kokokonin boisiek ng'ulek.*
*Si koribwech kisienyon bo kok si nyo kwomisien murenjun mengech.*
*Taing'ung ne lole bet ak kemo.*
*Profesa Lesan ko nyiganet ne kokikere sermosiek.*

*Tukitaka tujenge kaunti yetu hadi imetemete tunahitaji mtaalamu.*
*Profesa masomo yako ni sabuni ya*
*Kaunti ya Bomet.*
*Wazee wamekupatia mate.*
*Apate kutulindia sahani yetu ya wazee ili wanaume wale wengine wadogo waililie.*
*Taa yako inawaka usiku na mchana.*
*Profesa Lesan ni shujaa wetu ambaye tumemweka pembeni.*

*Ma kitisionin en ta yun.*
*Seneta nenyon ko moitumtumokse matiny.*
*Asi isoru bik en rubet kou Joseph en Egypt.*
*Digrii ing'ung ne itindoi ko kerge ak kiroki kibo Musa.*
*Si kotekisech murenchun.*
*Lesan ko long'enyon ne mi tai asi koik konyek.*
*Borienyon ak oret indochin ng'atutik kosibike ak long'et.*
*Kalyet en tai murenchu.*
*Kirgit choruandit ng'otut en boisiek.*
*Kirgit kosyinet kong'eten kuko ak baba.*

*Huwezi ukatishwa hata kidogo siku za usoni.*
*Seneta wetu hawezi kutingishika kamwe.*
*Waokoe walio na njaa kama Yusuf kule Misri.*
*Digrii uliyo nayo ni sawa na ile fimbo*
*Musa alikuwa nayo.*
*Ndipo wanaume wale wengine watatuheshimu.*
*Lesan ni ngao yetu aliye mbele yetu ili awe macho yetu.*
*Kabila letu na ukoo huongozwa na amri zikifuatana na ngao.*
*Tuweke amani mbele nyinyi wanaume.*
*Urafiki ni fahali na ni amri ya wazee wetu.*
*Maelewano ni fahali tangu enzi zile za mababu zetu.*

Whitehead (2003):4-aeleza kwamba suala la ubabedume hutegemea jamii husika. Ubabedume ni jinsi jamii yoyote huamini sifa zinazohusika na jinsia ya kiume na tabia za uume. Uume huhusu mazoea na njia zinazotumika kuthibitisha uume katika mwanaume au mvulana. Rangi, tamaduni, dini, mifumo ya imani, hali halisi ya mazingira na tajriba za kihistoria huchangia katika kuendeleza taasubi za kiume duniani hususan barani Afrika. Mawazo ya Whitehead yanalandana na maneno yapatikanayo katika wimbo ulioimbwa na Arumutik Kosgei. Msanii huyo alimtetea Profesa Lesan aliyekuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet 2017. Rejea sehemu ya wimbo ulio hapa juu.

Uchendu (1965) anatuarifu kuhusu maandishi ya Mouiche. Mouiche anatueleza jinsi bara la Afrika linaendeleza ubabe-dume na kusababisha ubaguzi wa kijinsia. Mageuzi ya hali ya kisiasa ya Waafrika na haki husika kimsingi, yalihamasishwa na ukoloni ambapo uliacha bara la Afrika na ubabedume uliokithiri. Mouiche alidhihirisha namna utawala wa kikoloni uliokuwa mkali, ulisababisha kuenea kwa ubabedume wa kisiasa baada ya ukoloni. Wakati wa utawala wa kikoloni, wanajeshi na hata wafanyikazi wengine walikuwa wa jinsia ya kiume. Kulingana na namna tumeelezewa na Uchendu juu ya ubabedume, hebu rejea wimbo ufuatao unaohusika na maelezo haya. Wimbo wenyewe uliimbwa na msanii aitwaye Titus Kosgei kuhusu Nathan Kirui aliyegombea kiti cha ubunge wa Bomet Mashariki. Katika wimbo huu, msanii alimwachia mgombezi kunena maneno machache kabla ya wimbo kuanza. Mgombezi alikuwa mwanaume na alinena kwamba kuingia kwake siasani, kulikuwa mwito wa kipekee. Yeye kama mwanaume, alifafanua mwenyewe kwamba alikuwa na imani na tumaini kubwa kuwa angepata kiti cha ubunge. Ndoto yake ilimwelekeza kwamba angefanya kazi pamoja na wenyeji na angewasikiza, angewasemea na kuwatendea. Msanii naye alimwinua Kirui akihamasisha wenyeji wamchague mwanaume chipukizi aliye shujaa na mwenye nguvu anayeweza kazi. Alifananisha mgombezi huyo na simba kuonyesha ujasiri, nguvu, msimamo na uwezo wake kama kiongozi kwa kutaja kwamba ni mwana wa Simba. Wimbo huu unausawiri uenezaji wa ubabedume, utawala wa jinsia uliokithiri katika jamii ya Wakalenjin. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Inoni ko kurset ne inegen.*
*Otinye kayanet en muguleldanyun.*
*Otinye komong'unet.*
*Inoni ko korwotitet ne inegen.*
*Otinye maketab keboisien tugul kibagenge.*
*Okoswok, omwoitewok ak oyoiwok.*
*Kikochin ra chito nyiganet neto koming'in Nathan Kirui.*
*Chitab bandab tai, kijanayat ne nomeke ak kasit.*
*Arwetab Simba, ki Simba kwanda.*

*Huu ni mwito wa kipekee.*
*Ninayo imani rohoni mwangu.*
*Ninalo tumaini.*
*Hii ni ndoto ya kipekee.*
*Nataka tufanye kazi pamoja.*
*Nawasikiza, nawasemea na kuwatendea*
*Tutampatia wakati huu mtu mpya, shujaa*
*wetu aliye chipukizi Nathan Kirui.*
*Ni mtu wa maendeleo, kijana chipukizi anayewezana na kazi.*
*Ni mwana wa Simba, baba yake alikuwa anaitwa Simba.*

Uchendu (2005) alifahamisha kuwa kwa ujumla, kulingana na vijana wa Nijeria, wanaume au wavulana huhusishwa na sifa fulani za kimwili, za kibiolojia na kisaikolojia kando na sifa za utu. Ifuatayo ni mifano ya sifa hizo: nguvu za kimwili, udhabiti, ujasiri, mwenye maamuzi, mwenye uwezo wa kulinda wanyonge, mwenye msimamo, mwenye uwezo wa kudhibiti, na anayeweza kuongoza. Mengi ya maelezo haya huonekana katika wimbo unaofuata ambao uliimbwa na msanii aitwaye Daniel Cheres. Alieleza wazi kwamba nchini Kenya tunao viongozi wapendanao wasioweza kutenganishwa hata kama siasa imechacha. Alikuwa akiwalenga Uhuru na Ruto kwa kufafanua kuwa Uhuru ni kama mti ulionawiri ambao umemea kando ya mto. Ruto ni tawi moja la mti huo na anatarajiwa ashike usukani Uhuru amalizapo kipindi chake cha utawala. Aliwashawishi wenyeji wautunze mti ipasavyo ili uendelee kustawi. Ruto aliyetajwa kama shujaa alishauriwa awalishe walio na njaa, watibiwe walioumizwa na wasiojiweza wasaidiwe. Kuungana pamoja kwa wanasiasa hawa wawili kunaonyesha ubabedume uliokithiri, tabaka ya utawala, msimamo na ujasiri wao kisiasa. Maana ya kupalilia mti ni namna wananchi walivyowaunga mkono wanasiasa hao wapate kuwa na nguvu thabiti na uwezo wa kuongoza nchi. Ruto alitarajiwa kuwalinda wanyonge kusawiri uwezo wake kama

mwanaume aliye kiongozi. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kitinye kondoik che makibestos.*
*Chame kalyet matiny komi bolet.*
*Orogendoen ketit ne mi tabandab oinet.*
*Ketit ne tinye temet neboe emet.*
*Temet ne tinye kimnatet, temoni ko nenyon Kalenjin.*
*Ongikutyin ng'ung'unyat temoni si ye kayosit keti ketinye ne nome boisiet.*
*Kiboe che ome rubet.*
*Kityoche che kigirat.*
*Kisobe che kikikoten.*
*Nyoru kiy che motinye kiy.*
*Osome toretet koyobun nyiganetab Kalenjin.*

*Tunao viongozi wasiotenganishwa.*
*Wanapenda amani hata kama kuna siasa.*
*Nafananisha na mti ulio kando ya mto.*
*Mti ulio na tawi linalolisha nchi.*
*Tawi lililo na nguvu, tawi hili ni letu Wakalenjin.*
*Tupalilie mti huu, halafu ukizeeka tutakuwa na wa kushika usukani.*
*Walio na njaa walishwe.*
*Waliofungwa wafunguliwe.*
*Watibiwe walioumizwa.*
*Wasio na chochote watapata.*
*Naomba usaidizi kutoka wewe shujaa wa Kalenjin.*

Mawazo makuu tuliyopewa na Uchendu, vilevile, hudhihirika katika wimbo ulioimbwa na msanii aitwaye Arumutik Kosgei aliyemtetea Shadrack Koech. Koech alikuwa akigombea kiti cha Ujumbe wa Wadi ya Obosi katika Kaunti Ndogo ya Ndanai 2017. Mgombezi huyo alikuwa akigombea kiti hicho kwa mara ya pili. Mwimbaji alimsifu akieleza kwamba yeye ni msomi na amepokelewa na wenyeji kuwa mjumbe wao wa Wadi. Alibarikiwa na wazee, vijana na kina mama. Walimfurahia kwa sababu hakukata tamaa aliposhindwa katika uchaguzi wa 2013. Mgombezi aliamua kuwa wadi hiyo ingeinuka kwani angeleta mabadiliko. Mgombezi alionyesha msimamo, ujasiri na nguvu zake kisiasa alipoamua agombee kiti hicho upya. Alisawiri uwezo wake na uamuzi aliponena kuwa angeleta mabadiliko katika wadi. Wenyeji walipompokea mwanaume huyo kugombea kiti hicho, inadhihirisha jinsi jamii huunga mkono na kuuendeleza ubabedume uliokithiri. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kisoman koyam somanet.*
*Kotoroch kokwenyin.*
*Iguitos tabusiek tugul chebo kasisiek.*
*Kirinemuge kong'eten 2012.*
*Kiimwa ile king'ete.*
*Ki kituiye vijana, boisiek ak chepyosok ak kekonin ng'ulek.*
*Imache iibu walet.*

*Alisoma ya kutosha.*
*Kijiji chake kimemlaki.*
*Anaelewa kazi atakazofanya.*
*Uligombea tangu 2012.*
*Ulisema tutainuka.*
*Tulikutana tukiwemo vijana, wazee na kina mama na kukubariki.*
*Unataka kuleta mabadiliko.*

**Itikadi ya Kisiasa kwa Jinsia ya Kike**

Hochschild (1989):257 aeleza kwamba wakati huu, hali ya uchumi imebadilika. Kuna kupunguka kwa uwezo wa kifedha hususan mshahara wa jinsia ya kiume, kupunguka kwa idadi ya kazi za wanaume zinazohitaji ustadi na zile zisizohitaji na kuongezeka kwa kazi za jinsia ya kike katika kanda za huduma. Wazo hili la Hochschild liko katika wimbo ulioimbwa na mwimbaji aitwaye Ben Bii. Alikuwa mtetezi wa marehemu Dkt. Laboso aliyekuwa akiwania kiti cha ugavana katika Kaunti ya Bomet na Beatrice Kones aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge wa Bomet Mashariki 2017. Katika wimbo wake anatufafanulia kwamba mambo ya kisiasa yanaenda kubadilika. Watu wa Bomet wameamua kubadilisha gavana na mbunge wa Bomet Mashariki wawe wa jinsia ya kike. Alieleza kuwa jambo hili ni la busara na yule asiyetaka kubadilika, dunia itambadilisha. Tendo kama hili litaleta ongezeko la kazi za jinsia ya kike kwenye kanda za huduma na kupunguza nguvu za ubabedume uliokithiri katika jamii. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Bikab Bomet Kounti ong'et kakoech*
*Kogeger konyone walet.*
*Dr. Joyce Laboso ne koketach koik Gavana.*
*Kiwole ra kele kiwole..*

*Kondoikyok ko kokelewen en chamaitab Jubilee.*
*Kokomwa kole kiwole.*
*Walaken ana komataikany si kewalin.*
*Ni ko tugetab ng'omnotet o papa..*

*Watu wa Kaunti ya Bomet mwamke kumekucha.*
*Tumeona mabadiliko yakija*
*Tumepokea Dkt. Joyce Laboso kuwa*
*Gavana.*
*Tutabadilisha wakati huu, tutabadilisha*
*Viongozi wetu wamechaguliwa katika Muungano wa*
*Jubilee*
*Wamesema tutabadilisha*
*Badilika au ungoje ubadilishwe*
*Hii ni sauti ya busara papa*

Wimbo ulioimbwa na Marion Chelang'at, unadhihirisha maelezo tuliyopewa na Hochschild. Mwimbaji huyo alikuwa akimtetea marehemu Laboso. Alifafanua kwamba watu walikuwa wanahitaji Laboso kuwa gavana kwani walitaka mabadiliko. Alieleza kuwa si lazima mwanaume atawale. Wanawake wapewe nafasi kisiasa na katika asasi nyingine za kijamii. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Omwochin Chemaluk chamat mising.*
*Ndandan kimoche chego, ko malazima kirgit.*
*Kimoche tuguk che lelach.*
*Ongele kiwole en Bomenyon.*
*Gavana ko Joyce, kamenyon korur bai.*
*Telel en sera che koimwa.*

*Mmwambie Chemaluk anapendezeka sana*
*Ingawa tunataka maziwa, si lazima tuwe na ndume.*
*Tunataka vitu vipya.*
*Mmwambie Chemaluk anapendezeka sana.*
*Gavana ni Joyce, mama yetu mwenye uwezo wa kulisha*
*jamii*
*Simama imara na sera zako ulizo nazo.*

Utawala wa wanawake kabla ya ukoloni kule Yorubaland, Hausaland na Igalaland ulileta changamoto kubwa kwa ubabedume katika jamii hizo. Walakini, kwa kurejelea Shokpeka (2002:111) anaamini kwamba kufanikiwa kwa utawala wa malkia wawili katika ufalme wa Benin, kabla ya ukoloni, kulitokana na mafanikio yao ya kiuchumi na utajiri wao. Baada ya utawala wao, uongozi wa kiume katika ufalme huo, uliondoa utawala wa wanawake. Waliamini kwamba kulingana na mila zao, 'wanawake hawakutambulika wakiwa wa hadhi ya juu katika jamii'. Wimbo unaofuata uliimbwa na Rodgers Mekenyo ambaye alitetea nguvu za mwanamke mgombezi aitwaye Luisa aliyegombea kiti cha Ujumbe wa Wadi 2013 na 2017. Msanii alieleza kuwa Luisa ana ujasiri, msimamo na uwezo wa kuongoza kwani akiingia siasani, anakuwa mshindi namna alivyofanya katika kinyang'anyiro cha 2013. Alimwinua akieleza kwamba alilinda wadi yake ipasavyo kwa kustawisha maendeleo. Aliwashauri wenyeji wampigie kura tena kwa vile hakuna kitu cha kufananishwa na mama. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Ongebirjin kura Luisa kityo.*
*Kongoi chepset lug ak kobor.*
*Kongoi Luisa chemaluk inyon.*
*Kongoi kamenyo koaba tany kot kekei.*
*Kongoi cherib gaa.*
*Kiritoret logokyyok ikochi 'basari'*
*Momi kit neu mama.*

*Tumpigie kura Luisa pekee.*
*Asante aendaye vitani na kuwa mshindi.*
*Asante Luisa wetu ambaye maziwa yake hayaishi.*
*Asante mama yetu akamuaye ng'ombe mpaka maziwa*
*yapatikane.*
*Asante mlinzi wa nyumbani.*
*Umewasaidia watoto wetu kwa kuwapatia 'bursary'.*
*Hakuna kinachofananishwa na mama.*

**MATOKEO**

Nyimbo kadha wa kadha ziliwatafutia wagombezi wapigaji kura kwa wingi. Wasanii walioimba nyimbo hizo waliwapigia debe wagombezi hao pamoja na vyama vyao wakitumia lugha ya kuvutia iliyoandamana na sauti zao pamoja na ala zao za muziki. Waliwaunganisha watu ili wafuate mkondo mmoja kisiasa na kuweko na upigaji wa kura ulio shwari. Miongoni mwa wasanii hao, kulikuwa na wale waliowachochea wagombezi wengine. Waliodhihakiwa hususan walikuwa wa jinsia ya kiume.

Kuambatana na nyimbo hizo, wagombezi wa kiume walipewa uwezo, hadhi ya juu na mamlaka hasa kulingana na nguvu zao za kimwili. Wasanii walieleza kwamba wao ni ngao walio na msimamo na wanategemewa pembeni. Walieleza kwamba

mwanaume anapaswa kuwa shujaa kama moto asiyeshtuliwa kwa ngozi. Yeye ni mwenye nguvu kwani anaweza kuinua mlima na hawezi kutingishika. Yeye amefananishwa na fahali na chuma. Anastahili kuwa kiongozi na mchungaji, yaani, macho au taa ya watu wengine. Wasanii waliwasifu wagombezi wa kiume kwa njia tofauti na wa kike. Mwanamke alisifika kama mama, mwanamke, mwangaza, mshindi na mtunzaji wa nyumbani kwake. Yeye ni mwenye uwezo wa kulisha jamii yake na ni yule anayependezeka. Inatupasa tumkumbuke mama kwani hakuna kitu kinachofananishwa naye kama wanavyofafanua wasanii. Kuna wasanii walioeleza kwamba kumekucha na tunataka mabadiliko na hata ingawa tunataka maziwa, si lazima tuwe na ndume.

Utafiti huu umefanikiwa kuonyesha kwamba nyimbo nyingi ziliunga mkono taasubi za kiume. Kwa kueleza kwamba mwanaume ni mfano wa moto, anaweza kumwua simba anayenguruma au hukinga pembeni, husawiri ujasiri, nguvu na uwezo wake mwingi. Hizi ni sifa hasa za kimwili zihitajikazo katika jambo gumu kama vita. Kwa sababu nyimbo hizi zilikuwa zikilenga siasa, inamaanisha kwamba siasa yenyewe imefananishwa na vita na kwa hivyo inahitaji mtu mwenye sifa kama hizi. Mwanamke hawezi kuhusishwa na sifa kama hizi katika jamii. Hapo ndipo mwanaume atapata nafasi ya kupanda ngazi kisiasa akijilimbilizia mali. Mwanamke hajapewa nafasi ya kutosha na jamii kufikia kiwango hicho. Matokeo haya yanadhihirisha kwamba jamii inakuza na kuendeleza ubabedume.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba nyimbo za kampeni za kisiasa zinafahamisha namna jamii huratibu majukumu kijinsia. Jambo hili hutokana na matarajio ya kiitikadi na utamaduni kuhusu jinsia zote mbili. Kuna sifa anuwai zinazomkweza mwanaume, jambo lililodumisha taasubi za kiume. Kumfananisha na watu maarufu katika Biblia kama Daudi, Musa na Yusufu ni namna ya kuujenga na kuupa nguvu zaidi ubabedume ulioshika mizizi duniani. Itikadi ya kisiasa kwa jinsia ya kike imesawiri mwanamke kama mama, mtunzaji wa nyumbani kwake, mwenye uwezo wa kulisha jamii yake, mwangaza na sifa nyingine zisizoakisi nguvu au uwezo wake hususan wa kimwili. Wasanii wachache waliutukuza ubabejike wakieleza kuwa kumekucha na mabadiliko yanahitajika. Jambo hili litafanikiwa iwapo litatiliwa mkazo na taasisi mbalimbali za jamii.

**Mapendekezo:** Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa jamii, kupitia nyimbo za kampeni za kisiasa, imeratibu majukumu ya kila jinsia. Hayo matokeo yamepatikana kupitia nadharia ya Ubabedume. Mtafiti apendekeza kwamba utafiti ufanywe zaidi kuchunguza namna ya kusawasisha uwezo wa mwanaume na mwanamke kupitia vyombo vingine vya kijamii.

**MAREJELEO**

Aswani, B., Mayaka, G., & Riro, M. (2014). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Carrigan, T., Connel, R., & Lee, J. (1985). Toward a new sociology of masculinity. In H. Brod (Ed.), *The making of masculinities: The new men studies*.

Commonwealth Observer Group. (2013). *Report of the Commonwealth Observer Group: Kenya General Elections*.

Connell, R. (1983). *Which way is up*. Sage Publications.

Connell, R. (1987). *Gender and power: Society, the person and sexual politics*. Sage Publications.

Connell, R., & James, W. M. (2005). Hegemonic masculinity: Rethinking the concept. *Gender & Society*. Routledge.

Deacon, D., Pickering, M., Golding, P., & Murdock, G. (1999). *Researching communications*. Arnold Ltd.

Fairclough, N. (1989). *Language and power*. Longman.

Fiske, J., Hodge, B., & Turner, G. (1987). *Myths of Oz: Reading Australian popular culture*. Allen and Unwin.

Hochschild, A., & Machung, A. (1989). *The second shift: Working parents and the revolution at home*. Viking.

Izugbara, C. O. (2005). Hypothesis on the origin of hegemonic masculinity. *Sexuality in African Magazine, 2*(1), 13–14. Africa Regional Sexuality Resource Centre.

Maclenness, J. (1998). *The end of masculinity*. Open University Press.

Sattel, J. (1983). Men, inexpressiveness, and power. In B. Thorne, C. Kramarae, & N. Henley (Eds.), *Language, gender and society* (pp. 119–124). Newbury House.

Shokpeka, S. (2002). Women in the history of pre-colonial Nigeria: The example of women in Edo State. *Nsukka Journal of the Humanities, 12*, 108–119.

Simatei, P. (2010). Kalenjin popular music and the contestation of national space in Kenya. *Journal of Eastern African Studies, 4*, 425–434.

Uchendu, V. (1965). *The Igbo of south-eastern Nigeria*. Holt, Rinehart and Winston.

Uchendu, E. (2005). Masculinities from perspectives of youth. Paper presented at the Gender Institute–CODERSIA.

Wamitila, K. W. (2003). *Folk literature*. Focus Publication.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.

Whitehead, S. M. (2003). *Men and masculinities: Key themes and new directions*. Blackwell Publishers.